

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**



**Taarifa ya Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa  
Nape Moses Nnauye, katika kuadhimisha Siku ya TEHAMA Afrika, tarehe 7,  
Desemba 2022**



*Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb.)*

---

Salaam!

Mnamo tarehe 7 Desemba 1977 huko Addis Ababa, Ethiopia, katika kikao cha Kumi na Mbili (12) cha Wakuu wa Nchi na Serikali wanachama wa Umoja wa Muungano wa Afrika (OAU) walianzisha Shirika la Mawasiliano la Wanamajumui wa Afrika (PATU) lililoasiwa kama wakala maalum wa Umoja huo kwa sasa ukijulikana kama Umoja wa Afrika (AU) ili kusimamia sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Ilipowadia tarehe 7 Desemba 1999, PATU ilihuisha jina lake na kuwa Shirika la Mawasiliano Afrika (ATU) ambalo linaitambulisha taasisi hiyo hadi hivi leo.

Tangu wakati huo, kila inapowadia tarehe 7, Desemba, Afrika imekuwa ikiadhimisha siku ya ATU au siku ya TEHAMA kama kumbukizi ya kuasiwi kwa Shirika hili muhimu katika usimamizi wa sekta ya Mawasiliano barani Afrika. Mwaka huu ATU inaadhimisha miaka 45 ya kuasiwi kwake; Tanzania kama mwanachama hai wa Shirika hili, inaungana na nchi nyingine wanachama katika kumbukizi hii muhimu ambayo ni siku ya TEHAMA kwa bara la Afrika.

Ndugu wadau, Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine wanachama wa Umoja wa Afrika na Shirika la Mawasiliano Afrika (ATU), imekuwa mwanachama hai na mwenye mchango chanya katika kukuza Maendeleo endelevu ya sekta ya mawasiliano na TEHAMA. Na

kwa kuzingatia dhima ya maadhisho ya mwaka huu isemayo "**Kukuza Uchumi Shirikishi kupitia TEHAMA**", na mikakati mbalimbali ya ki-nchi na ki-Sera inayoendelea kuchukuliwa, tunayo imani kubwa kwamba, tutafanikiwa na kufikia lengo la kujenga na kukuza uchumi *wezeshi na shirikishi* kupitia TEHAMA na mifumo mingine bayana ya Kidijitali ili kumnufaisha kila Mwananchi, biashara na sekta nzima ya uchumi wa nchi na bara la Afrika.

Kama nchi, tunatambua kuwa, ujumuishi wa upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wetu ni kichocheo muhimu ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Ufikiwaji wa huduma za kifedha kwa wote na Mkakati wa kupunguza umaskini (SDG 1) kupitia fursa za ajira na biashara zinazozalishwa kupitia mifumo ya Uchumi wa Kidijitali. Serikali imekuwa ikihakikisha dhana ya 'uchumi jumuishi kupitia mifumo ya kidijitali' inakuwa halisi. Suala hili tunalitekeleza kwa vitendo!, na hatua za sasa ni kuhakikisha ufikiwaji wa huduma za intaneti unakuwa wa uhakika kwa wote ili uwezeshe kukuza uchumi jumuishi wa Kidijitali.

Ili kuhakikisha lengo la ufikiwaji wa huduma za Mtandoa hasa wa intaneti linakuwa halisi na kamilifu, uimarishaji na Ujenzi wa miundombinu thabiti na ya uhakika ya Mawasiliano hasa Mawasiliano ya intaneti ni muhimu. Tunaendelea na kazi ya kuunganisha mikoa yote na wilaya zote za Tanzania kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB) ambapo hadi sasa tumekamilisha Ujenzi wa Mkongo kwa takribani Kilomita 8,319, lengo likiwa kuunganisha mikoa, wilaya na maeneo yote ya mipaka ya nchi zikiwemo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, DRC, Zambia, Mozambique na Malawi. Kazi ya kuunganisha mikoa yote imekamilika na sasa tunaunganisha wilaya zote ili wananchi wanufaike na huduma za kifedha kwa njia ya Mtandoa kupitia huduma za mkongo.

Uchumi wa Kidijitali ambao kwa asilimia zote ni uchumi jumuishi unafanikiwa na utafanikiwa kwa kuhakikisha miundombinu hii ya Mkongo wa Mawasiliano inakamilika. Sisi kama wizara yenye dhamana ya Mawasiliano na mifumo ya TEHAMA tumejidhatiti kuhakikisha mifumo na miundombinu ya Mawasiliano inakamilika ipasavyo. Mbali na mkakati wa kujenga mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pia tutahakikisha Vituo vya kisasa vya Taifa vya Kuhifadhi Data za Mtandoa wa Mawasiliano vinakamilika na kufikika kwa ajili ya kutoa huduma ya kuhifadhi Taarifa zikiwemo za uchumi kwa watumiaji huduma za uchumi wa Kidijitali.

Wakati nikihitimisha kauli hii, ningependa kuweka bayana kwamba Serikali imeweka lengo la kufikisha asilimia 80 ya huduma ya Mtandoa wa intaneti hadi ifikapo mwaka wa 2025. Lengo letu ni kuhakikisha tunakuwa na Sera na Sheria Rafiki kwa sekta, tunajenga miundombinu thabiti ya Mawasiliano kama vile Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na vituo thabiti vya kuhifadhi data, kuwa na mifumo na Taasisi rafiki kwa sekta ili kuiwezesha kukua na kuwa na mifumo Madhubuti ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika sekta

ya Mawasiliano na TEHEMA ili kuendana na mifumo ya kimataifa iliyokubaliwa katika kufikisha huduma za kiuchumi kwa wote kuitia njia za Mawasiliano yaliyoboreshwa.

**Heko ATU kwa kuadhimisha miaka 45.**